**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA KILIMO**

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA**
**NAFAKA NA MAZAO MCHANGANYIKO**

## TAARIFA KWA UMMA

## UTOAJI WA VIBALI VYA MAZAO YA MAHINDI NA MCHELE

**17 APRILI 2025**

Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA) imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Usalama wa Chakula Sura 249 na marekebisho yake yaliyofanywa kupitia Sheria ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko Sura 274. Kwa mujibu wa kifungu cha 4 (1) (h) cha sheria hiyo, mojawapo ya majukumu ya Mamlaka kutoa vibali vya kutoa nje ya nchi na kuingiza ndani ya nchi, nafaka na mazao mchanganyiko, na kumshauri Waziri mwenye dhamana ya Kilimo juu ya mwenendo wa hali ya mazao hayo nchini.

Katika kutimiza majukumu hayo, COPRA inatarajia kufanya tathimini ya kina ya hali ya upatikanaji wa mazao ya mahindi na mchele nchini. Tathmini hiyo itahusisha, kupata taarifa ya kiasi cha mazao hayo kilichopo nchini, maoteo ya uzalishaji wa msimu wa 2024/2025 na upatikanaji wa chakula kwa mwaka 2025/2026 pamoja na taarifa za kiasi cha mazao hayo kilichosafirishwa kwenda nje ya nchi. Zoezi hili linatarajiwa kuanza tarehe 1 Mei 2025.

Hivyo basi, COPRA inautangazia Umma kuwa vibali vya kusafirisha mahindi na mchele vitaanza kutolewa baada ya kumalizika kwa tathimini hiyo. Wafanyabiashara wanashauriwa kutumia vibali ambavyo vimetolewa na Mamlaka ndani ya mwezi wa Aprili, 2025. Vibali vyote ambavyo vitakua havijatumika hadi tarehe 30 Aprili 2025 vitasitishwa na havitatambuliwa kwenye mfumo wa usafirishaji wa mazao hayo.

Imetolewa na,

**MKURUGENZI MKUU**

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA NAFAKA NA MAZAO MCHANGANYIKO**

*Jengo la Kahawa Plaza, Mtaa wa Njedengwa, S.L.P 2780, Dodoma -Tanzania.*

*Simu: 0800 11 77 77 , Barua pepe: info@copra.go.tz.*